


OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA MANISPAA YA UBUNGO
SHULE YA SEKONDARI TEMBONI GVT
S.L.P 90304, REG; 2355.SIMU +255 755 013 911
DAR ES SALAAM,



JINA LA MWANAFUNZI:

FORM YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2023.

Uongozi wa shule ya Sekondari **TEMBONI GVT** Unayo furaha kujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka 2023 katika shule ya Sekondari **TEMBONI GVT** kama mwanafunzi wa kutwa. Hongera sana kwa kupata nafasi hii adimu.

MAHALI SHULE ILIPO:

Shule ya Sekondari **TEMBONI GVT** ipo mkoa wa Dar es Salaam, Wilaya ya **Ubungo**, Kata ya **MSIGANI** mtaa wa **MSINGWA** jirani na shule ya Msingi Temboni. Umbali kutoka barabara kuu kufika shulenii kilometra **4.5**. Usafiri unaopatikana kutoka barabara kuu (Morogoro road) kituo cha kwa msuguli hadi shule ni Bajaji na Pikipiki .

MUDA WA KUFUNGUA SHULE

Mwanafunzi anatakiwa kufika shule akiambatana na mzazi wake tarehe **09/01/2023** Saa 1:00 asubuhi fika na Fomu ya usajili pamoja na vitu vyote vinavyohitajika ili uweze kusajiliwa. Mwanafunzi ambaye hataripoti kwa muda uliopangwa, nafasi yake itajazwa na mwanafunzi mwingine.

MAHITAJI MUHIMU YA KUJA NAYO SHULENI

1. Sare ya Shule
2. Begi la kubebea madaftari Jeusi la mgongoni.
3. Mkebe wa vifaa vya hisabati
4. Madaftari 11 counter book (Quire 3 au 4)
5. Kamusi (Dictionary) **English to English**.
6. Mathematical four figure table
7. Graph pad
8. Kalamu ya wino na risasi pamoja na rula
9. T-shirt , bukta ya rangi dark blue, raba nyeupe zisizo na shingo ndefu kwa ajili ya michezo.
10. Vitabu viwili vya kiingereza, ambavyo ni (i) Mabala the Farmer (ii) Hawa the Bus Driver.

MAELEZO YA SARE YA SHULE:-

WAVULANA

- Shati jeupe (tomato)la mikono mifupi lisilo bana pair mbili 2.
- Suruali ya rangi **NYEUSI** yenye upana wa inchi 17 chini na marinda mawili kila upande pea (2) mbili (isiwe modo) na Tai pea mbili (2) kufuatana na rangi ya suruali
- Soksi ya rangi nyeusi pair mbili (2)
- Viatu vya ngozi vyeusi vya kufunga na kamba visivyo na kisigino (sio raba wala buti).
- Nywele fupi sio kipara
- Mwanafunzi awe na saa ya mkononi.
- Mkanda wa ngozi mweusi .

WASICHANA

- Mashati meupe (tomato)mawili ya mikono mifupi yasiyo bana.
- Sketi ya rangi **NYEUSI** ya marinda box, ndefu kupita magoti pair mbili (2) na tai mbili (2)kufuatana na sketi
- Soksi za rangi nyeupe pea mbili (2)
- Viatu vyeusi visivyo vya kisigino vya kufunga na kamba vya ngozi (sio simple wala juma na roza)
- wasichana wanao vaa hijabu wanatakiwa kuva sketi ndefu .
- Wasichana wanatakiwa kuva nusu kanzu na iwe na mikono mirefu ya kutosha isiyobana .
- Nywele fupi sio kipara
- Mwanafunzi awe na saa ya mkononi.

SHERIA ZA SHULE,Nidhamu kwa ujumla

1. Ni lazima mwanafunzi awahi shulenii asubuhi saa 1:00 na kufanya usafi wa mazingira ya shule na kuhudhuria gwaride la ukaguzi wa usafi na kuchangamsha mwili.
2. Mwanafunzi ye yote haruhusiwi kuondoka katika eneo la shule bila kupata kibali kutoka kwa mwalimu wa darasa, wa zamuu au idara ya malezi.
3. Mwanafunzi anatakiwa kusimama, kusalimia na kuwapokea mzigo walimu au mtu ye yote mwenye umri mkubwa zaidi yake popote pale akutanapo na watu wa aina hiyo.
4. Hairuhusiwi kutumia **LUGHA CHAFU** miiongoni mwa wanafunzi na kwa mtu mwingine ye yote.
5. Mwanafunzi anatakiwa kuwaheshimu wanafunzi wenzake, viranja na wafanyakazi wote wa shule.
6. Kila mwanafunzi ni lazima ahudhurie vipindi vyote vya darasani na shughuli za michezo, na uzalishaji mali kwa mujibu wa ratiba.
7. Mwanafunzi lazima afanye mitihani ya masomo yote anayosoma shulenii hapa.
8. Mwanafunzi awapo shulenii haruhusiwi kuwa na aina yoyote ya vitu vifuatavyo:- Kucha ndefu, kupaka rangi, kuva cheni, hereni, nywele ndefu, kunyoa kipara, kunyoa nyusi, kupaka dawa nywele,kunyoa nywele mtindo wowote n.k.
9. Mwanafunzi ahakikishe kuwa awapo mahali popote ndani au nje ya shule awe amevaa nguo za heshima. Ni marufuku kuva nguo zinazobana, fupi na nyepesi.
10. Mwanafunzi haruhusiwi kuja na nguo zaidi ya zile zilizotajwa katika maeleo ya kuijunga na shule, ikiwemo sweta la rangi ya kijani ya jeshi kwa anayetaka.
11. Wanafunzi wanatakiwa kutunza mali zao binafsi na mali za shule. Pia wanatakiwa kutoa taarifa kwenye utawala juu ya uharibifu wa mali ya shule.
12. Ni marufuku kwa mwanafunzi yoyote kwenda kwenye maeneo yafuatayo bila sababu maalumu au bila kupewa ruhusa:-
 - I. Shule za jirani na madukani .II. Nyumba zinazozunguka shule na III. Vibanda vya biashara nje ya shule
13. Ni marufuku kwa mwanafunzi kukutwa sehemu zifuatazo:-
 - I. Baa na klabu za usiku.
 - II. Nyumba za kulala wageni isipokuwa wanapokuwa na wazazi au walezi wao
14. Wawapo shulenii wanafunzi hawaruhusiwi kumiliki vitu vya gharama kama: Simu ya mkononi, redio, kamera, ipad, albam za picha na CD.
15. Kila mwanafunzi ni lazima afanye bidii katika kila somo. Mwanafunzi ambaye atapata alama chini ya 50% mwisho wa mwaka atakariri darasa (atarudia).
16. Hakikisha ukimya wa hali ya juu unazingatiwa katika maeneo yote ya shule nay a kujifunzia hasa darasani, maktaba, maabara na kwenye koridos wakati wa vipindi.
17. Adhabu ya viboko itaruhusiwa kwa kosa linalostahili na kuwa na taarifa/ kibali cha mkuu wa shule.
18. Hakikisha muda wote unapokuwa shulenii unaongea lugha ya kiingereza nje na ndani ya darasa.
19. Mwanafunzi ye yote akikamatwa na kitu chochote kisichotakiwa shulenii kitaharibiwa mbele yake.
20. Hairuhusiwi kuruka uzio ukikamatwa utalipa uzio rola moja (waya wa kashata) na kugharamia ufundi.

B. MAKOSA AMBAYO MWANAFUNZI AKIFANYA ANAWEZA KUFUKUZWA SHULE.

1. Kutochukuwa ripoti ya maendeleo yake ya nusu mwaka au mwaka.
2. Ulevi au matumizi ya madawa ya kulevya.
3. Aina zote za wizi na unyang'anyi.
4. Aina zote za makosa ya kujamiana na uasherati. Hii ni pamoja na kukutwa na mikanda ya video, vitabu vichafu vya uasherati au vitu vinavyofanana na hivyo.
5. Kupiga au kupigana.
6. Matumizi ya lugha chafu zu matusi.
7. Makosa ya jinai.
8. Kuzomea watumishi au kuchokoza wanafunzi wengine.
9. Kugoma au kuchocha mgomo (ghasia)
10. Kutohudhuria shulen i kwa muda wa siku 30 mfululizo bila taarifa.
11. Kudharau Bendera ya Taifa kwa kutohudhuria paredi.
12. Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule, (Pia ikithibitika kutoa mimba)
13. Kuoa au kuolewa
14. Kukuwadia mwanafunzi mwenzie na mtumishi yejote katika mambo ya mapenzi ndani na nje ya shule.
15. Kunyanyasa mwanafunzi mwenzie kutokana na jinsia yaek, udini, ulemavu, ugeni wake au hali yake.
16. Kughushi mitihani au wizi wa mitihani , kukataa au kutofanya mitihani na mazoezi ya masomo bila sababu za msingi.
17. Kukataa adhabu kwa makusudi. Pia adhabu inaweza kutolewa na mwalimu au kiranya yejote kwa mwanafunzi anayeonesha utovu wa nidhamu.
18. Kuharibu mali ya shule ikiwa ni pamoja na majengo, mali ya mtu au kundi la watu.
19. Kukamatwa na simu , redio kamera, ipad albam za picha na CD mara ya pili baada ya kuonywa kwa mara ya kwanza.
20. Kuruka uzio.

C. WAJIBU WA MZAZI

1. Mzazi/ Mlezi anatakiwa kumleta mwanae kumwandikisha shulen anapoanza masomo.
2. Mzazi /Mlezi anatakiwa kuandikisha majina ya watu wawili na namba zao za simu watakoruhusiwa kupata ripoti za mtoto na mawasiliano ya vikao, wito n.k
3. Mzazi /Mlezi anatakiwa kuja kuchukua ripoti ya mtoto wake kwa muhula husika vinginevyo hatapokelewa muhula unaofuata.
4. Mzazi /Mlezi anatakiwa kufika shulen kwa muda muafaka pindi anapohitajika na uongozi wa shule.
5. Mzazi/ Mlezi amfahamu kwa jina na achukue namba ya simu ya mwalimu wa darasa la mtoto wake ili kujenga mahusiano ya malezi ya mtoto.
6. Mzazi /mlezi ajenge tabia ya kutembelea shule mara kwa mara ili kujua maendeleo ya mtoto wake badala ya kusubiri kuitwa ili kujenga mshikamano wa malezi.

KARIBU SANA KATIKASHULE YETU.

.....
NOAH R. BALLIGE
MKUU WA SHULE

MUHIMU:

Fomu zilizoambatanishwa zinatakiwa zijazwe kikamilifu na zirudishwe shulen.

1. Fomu rasmi ya kuandikishwa
2. Ahadi ya mwanafunzi na Mzazi/Mlezi.
3. Fomu ya uchunguzi wa Daktari.

KIAMBATANISHO ‘A’

FOMU RASMI YA KUANDIKISHWA

Sehemu hii Ijazwe na mwanafunzi:-

1. Jina kamili la mwanafunzi:
2. Uraia:
3. Dini:
4. Tarehe ya kuzaliwa:
5. Mahali ulipozaliwa: Mahali anapoishi Kata.....
6. Yatima / Sio yatima / mzazi mmoja (Kata isiyohusika)
7. Shule uliyosoma kabla ya kuja Sekondari ya.....(Jaza jedwali)
8. Aina ya usafiri anaotumia miguu, gari moja , gari mbili , gari tatu.

Picha

JINA LILIOANDIKISHWA SHULENI	SHULE YA MSINGI/SEKONDARI ULIKOTOKA	MWAKA ULIOANZIA	MWAKA ULIOTOKA

Saini ya mwanafunzi Tarehe

Sehemu hii ijazwe na Mzazi / Mlezi

- (1) Jina kamili la Mzazi / Mlezi
- (2) Uraia
- (3) Anuani kamili mjini DSM
- (4) Sehemu unayoishi Wilaya
- (5) Mtaa
- (6) Kata
- (7) Namba ya simu(ya haraka)

Maelezo ya kikazi ya Mzazi / Mlezi

1. Jina la mwajiri na idara
 2. Anuani
 3. Namba ya simu
 4. Kazi ya mzazi / mlezi
- (mfano; karani , Meneja, Mwalimu, Mfanyabiashara n.k)

Saini ya Mzazi / Mlezi Tarehe :

Majina mawili ya ndugu /Mlezi wa mwanafunzi

Picha

S/NO	JINA	UHUSIANO	NAMBA YA SIMU
1.			
2.			

**KIAMBATANISHO ‘B’
E. FOMU YA AHADI.
AHADI YA MWANAFUNZI**

Mimi

1. Nimeyasoma na kuyaelewa maelekezo yote na nimekubali kujiunga na shule hii ya Sekondari ya kuanzia tarehe
2. Naahidi kwamba:-
 - (a) Nitazingatia Sheria zote za shule na kutimiza mambo yote muhimu yaliyotajwa .
 - (b) Sitashiriki katika vitendo vya hujuma wala vitendo ambavyo vitakuwa kinyume na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
 - (c) Nitatunza mali ya umma ambayo ni pamoja na Majengo , Samani , vitabu na vifaa vya maabara.
 - (d) Nipo tayari kuchukuliwa hatua yoyote stahiki endapo nitakiuka maelezo yaliyotolewa kwenye fomu hii.

Saini ya mwanafunzi Tarehe :

.....

AHADI YA MZAZI / MLEZI

Mimi

Mzazi / Mlezi wa kidato..... Naahidi kwamba:-

- a) Nitashirikiana kikamilifu na uongozi wa shule na walimu wote kwa ujumla katika kumwelimisha na kumlea mtoto wangu. Hii ni pamoja na kuhakikisha kuwa atazitii sheria zote za shule na kuyatimiza yote muhimu yaliyotajwa.
- b) Nitafanya kila niwezalo kumwezesha mwanangu kufika shulenii kila siku kabla ya saa 1:00 asubuhi
- c) Na kwamba mwanafunzi atahitimu na kufuzu kidato cha kwanza hadi cha nne.
- d) Ninaruhusu mwanangu achukuliwe hatua yoyote stahiki endapo atavunja mojawapo ya sheria na kanuni zilizoorodheshwa.

Saini ya mzazi / mlezi Tarehe:

**THE UNITED REPUBLIC OF TANANIA
PRESIDENT OFFICE
REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
TEMBONI GVT SECONDARY SCHOOL**

Request for Medical Examination

To be filled by Government Medical Officer and return to the Head of TEMBONI GVT Secondary School, P.O.BOX 90304. DAR ES SALAAM.

To the Medical Officer,

.....
.....

A. Re

Please examine the above mentioned student comment on his/her fitness by responding to the problems below say YES or NO each problems and if YES then state.

Signature

HEADMASTER.

Date

Insert (V) in the boxes provided

i.	Hearing	YES (<input type="checkbox"/>)	NO (<input type="checkbox"/>)
ii.	Speech	YES (<input type="checkbox"/>)	NO (<input type="checkbox"/>)
iii.	Sight	YES (<input type="checkbox"/>)	NO (<input type="checkbox"/>)
iv.	T.B	YES (<input type="checkbox"/>)	NO (<input type="checkbox"/>)
v.	B.T	YES (<input type="checkbox"/>)	NO (<input type="checkbox"/>)
vi.	Diabetes	YES (<input type="checkbox"/>)	NO (<input type="checkbox"/>)
vii.	Mental case	YES (<input type="checkbox"/>)	NO (<input type="checkbox"/>)
viii.	Physical disability	YES (<input type="checkbox"/>)	NO (<input type="checkbox"/>)
ix.	Any	YES (<input type="checkbox"/>)	NO (<input type="checkbox"/>)

Destination

Signature Date